

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA NANE

28 APRILI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA NANE – TAREHE 28 APRILI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA KILIMO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

203. MHESHIMIWA JOHN FRANCISCO NZILANYINGI (NYAMAGANA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali inampango gani wa kujenga Barabara za pembezoni na Mtaani maeneo ya Kushiri, Mahina, Luchelele na Lwanchima.

204. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakarabati Shule ya Msingi Mtapenda Kata ya Mtapenda - Nsimbo.

205. MHESHIMIWA DEVOTHA DANIEL MBURARUGABA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ipo tayari kutenga dirisha maalum la Mikopo kwa Sekta za kipaumbele za Kilimo cha Kahawa, Ufugaji na Biashara ndogondogo - Kagera.

206. MHESHIMIWA PATALI SHIDA PATALI (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Soko la uhakika la mazao Mbeya Vijijini.

OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

207. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Kada ambazo hazipo kwenye orodha ya Kada za Sekretarieti ya Ajira kwa kuwa zinafundishwa Vyuoni.

WIZARA YA NISHATI:

208. MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MTAMA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ipo tayari kuweka wazi Mpangokazi wa mwelekeo wa mazungumzo juu ya Mradi wa LNG - Lindi kwa kuwa umechukua muda mrefu.

209. MHESHIMIWA INNOCENT LUGHA BASHUNGWA (KARAGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Umeme katika Shule za Sekondari, Msingi na Taasisi zote za Wilaya ya Karagwe.

WIZARA YA UJENZI:

210. MHESHIMIWA KASSIMU AMARI MBARAKA (TANGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Kiomoni, Pande, Mjesani hadi Muheza inayounganisha Wilaya ya Tanga na Muheza utaanza.

211. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Km 23 kutoka Mlandizi hadi Ruvu *Station* (SGR) kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

212. MHESHIMIWA EDIBILY KAZALA KINYOMA (KASULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itamaliza changamoto ya Mawasiliano kwa kujenga Minara Kata za Heru Ushingo, Kagerankanda na Asante Nyerere - Kasulu Vijijini.

WIZARA YA FEDHA:

213. MHESHIMIWA DICKSON NATHAN LUTEVELE (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa Kodi ya 30% katika *export* ya Mazao ya Mimitu ambayo imeua kabisa Viwanda.

WIZARA YA KILIMO:

214. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Skimu za Umwagiliaji katika Mkoa wa Kilimanjaro.

**215. MHESHIMIWA ZUBERI YAHYA MFAUME
(MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Wakulima wa ufuta wa Kisaki, Mvuha, Mngazi, Bwakila chini na Selebala waliouza kwa Mfumo wa Stakabadhi ghalani watalipwa fedha zao.

WIZARA YA UCHUKUZI:

**216. MHESHIMIWA KIZA HUSSEIN MAYEYE (KIGOMA
KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Wananchi wa Kigoma watanufaikaje na Mkataba baina ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na Kampuni ya Zijini ya China kuendesha Bandari ya Kigoma.

WIZARA YA MAJI

**217. MHESHIMIWA ENG. FADHILI SANDALI CHILOMBE
(TUNDURU KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Miradi ya Maji katika Jimbo la Tunduru Kusini.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA KILIMO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA
28 APRILI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**

